



MWANAMKE, KWA NINI UNALIA? NA MARK R. PUGH

### Mashahidi Wengi wa Ufufuko Wake

“Ninaamini mashahidi wengi wa Ufufuko wa Mwokozi ambao nuzoefu na shuhuda zao hupatikana katika Agano Jipya—Petro na wenza wake wale kumi na wawili na mpendwa, msafi Mariamu wa Magdala, miongoni mwao. Ninaamini shuhuda zinazopatikana katika Kitabu cha Mormoni—wa Nefi Mtume pamoja na umati ambao hawakutajwa majina katika Bountiful, miongoni mwao. Na ninaamini ushuhuda wa Joseph Smith na Sidney Rigdon ambao, baada ya shuhuda nyingine nyingi, walitangaza ushahidi mkuu wa kipindi hiki cha mwisho cha mwongozo wa Mungu ‘kwamba yu hai! Kwani tulimuona.’ Chini ya mtazamo wa uoni wote wa jicho Lake, ninasimama mwenyewe kama shahidi kwamba Yesu wa Nazareti ni Mkombozi aliyefufuka, na nina-shuhudia kwa yote yatakayofuata kutoka kwenye *ukweli* wa Ufufuko Wake. Na upokee usadikisho na faraja ya ushahidi kama huo.

Mzee D. Todd Christofferson wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili, “Ufufuko wa Yesu Kristo,” *Liahona*, Mei 2014, 114.

**Matumizi Binafsi:** japokuwa hatukuwa kati ya wale waliouona mwili uliofufuka na mkamilifu wa Mkombozi, bado tunaweza kusimama kama mashahidi Wake leo. Yeye daima anaweza kuwa lengo la maisha yetu, bila kujali muda au mahali tunapojikuta. Kila mara tunapotoa mioyo na mikonno yetu kuwatumikia wengine; kuonyesha upole, ukarimu, na heshima kwa wote; kutetea ukweli; na kutoa shuhuda zetu za injili, tunasimama kama mashahidi wa kweli wa Yesu Kristo.

UTONDOTI KUTOKA WALK WITH ME, NA GREG OLSEN, YASINAKILIVE

### Hatuna Haja ya Kutembea Peke Yetu

“Mojawapo ya faraja kuu ya kipindi hiki cha Pasaka ni kwamba kwa sababu Yesu alitembea njia hiyo ndefu ya upweke kabisa peke yake, *sisi* hatuhitaji kufanya hivyo. Safari yake ya upweke ilileta umoja mkubwa kwa tafsiri yetu ndogo ya njia ile—utunzaji wa rehema wa Baba Yetu wa Mbinguni, wenza usioshindwa wa huyu Mwanawe Mpendwa, kipawa kikamilifu cha Roho Mtakatifu, malaika walio mbinguni, wanafamilia pande zote mbili za pazia, manabii na mitume, walimu, viongozi, marafiki. Vyote hivi na zaidi vimetolewa kama wenza kwa safari yetu ya maisha ya duni-ani kwa sababu ya Upatanisho wa Yesu Kristo na Urejesho wa injili Yake. Ukitangazwa kutoka kilele cha mlima Kalvari ni ukweli kwamba kamwe hatutaachwa peke yetu wala bila msaada, hata kama wakati mwingine tunaweza kuhisi tumeachwa. . . .

“ . . . Na tusimame na Yesu Kristo ‘nyakati zote na katika mambo yote, na mahali popote [tulipo], hata hadi kifo,’ kwani hakika hivyo ndivyo alivyosimama nasi wakati ili *kuwa* katika kifo na alipotakiwa kusimama kabisa peke yake.”

Mzee Jeffrey R. Holland wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili, “Hakuna Aliyekuwa Pamoja Naye,” *Liahona*, Mei 2009, 88.

**Matumizi Binafsi:** Pasaka Hii, kumbuka safari ya mwisho ya Mwokozi, safari ya upweke. Alijitolea kila kitu alichokuwa nacho ili kwamba wewe na kila mtu duniani aweze kuwa msafi na kupata uzima wa milele. Jifunze kutokana na mfan-ano Wake mkamilifu. Muweke katika mawazo yako na katika moyo wako. Na daima kumbuka kwamba kamwe hauko peke yako. Kwa sababu alivumilia safari Yake ya mwisho kwa ukamilifu wa kipekee, Yeye hatakuacha. Upendo Wake kwako hauna mwisho na haubadiliki, na anasimama tayari kukupatia amani, faraja, na tumaini unapoendelea katika safari yako mwenyewe. Zawadi yake ya Upatanisho haina mwisho, na ilitolewa kwako. ■

Ona jinsi Pasaka ya Wayahudi inavyotusaidia kuelewa Pasaka kwenye [lds.org/go/41817](https://www.lds.org/go/41817).

